

Misingi Iliyo Imara

Warumi 1:16 inasema, “Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye: kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.”

Mungu anaweza na anafanya kazi kwa njia nyingi. Kikubwa zaidi anafanya kazi pamoja na kupitia watu wake, akiwaalika kusema na kuwaonyesha wengine habari njema za Yesu: Injili. Habari hizi njema zina nguvu, ikileta tumaini na maisha mapya, ikiwaokoa watu toka maisha ‘yaliyokufa’. Inapendeza kuwa Mungu anatumia kuwashuhudia watu habari hizi njema! Msingi wetu uliyo imara uko ndani ya MUNGU kufanya kazi pamoja nasi, na kupitia sisi watu wake.

Kwenye kitabu cha Isaya 61:1-4, tunasoma kuwa wokovu wa Mungu huwaweka watu huru kiroho, kihisia, na kimwili. Hebu tazama hivyo vifungu mwenyewe na ugawanye matendo kwenye aina 3: kiroho, kihisia na kimwili.

Utugundua kuwa ni Roho wa Bwana (k1) anafanya kazi pamoja na hao waliowekwa huru (k3). Mungu anawaita watua hao ‘mwaloni (miti mikubwa) ya haki’. Hii ni picha nzuri sana Mungu akifanya kazi na watu wake kuleta uhuru na uponyaji. Lengo la Mungu ni kurejesha vitu vyote. Mahali dhambi imeharibu dunia yetu na maisha yetu, anataka kufanya vitu vyote kuwa mpya na kamili tena.

Kama watu wa Mungu, tunapaswa kuchakua kama tutaishi kama ‘mwaloni ya haki’ kwenye jumuia zetu, tukiwa na ushirika na Mungu. Tunapofanya hivyo, wengine pia watawekwa huru na kupandwa karibu nasi. Kwa pamoja tunafanyika utukufu wa Mungu. Tukiingiza hiyo kwenye kijiji chetu, ina maana kuwa watafanyika mahali salama, huru yenye kupendeza.


Huu ni msingi wetu uliyo imara. Mungu anatumia sisi tufanyike sehemu ya kazi yake kuwaokoa watu kupitia nguvu ya injili! Habari njema za Yesu italetwa uponyaji, haki na matumaini kwenye jumuia yetu. Bado Mungu kuingia kwenye vijiji vyetu hutegemea kutaka kwetu kushirikiana naye kwa kushuhudia na kuonyesha habari njema ya Yesu kuleta uzima kwa kila moja.

Omba:

- 1) Mungu atakuonyesha maono yake kwa jumuia yako.
- 2) Someni pamoja kwa maombi Isaya 61:1-4. Mwalike Mungu akuangazie mstari uliyo wa muhimu kwa kijiji chako muda huu. Kwa mfano, anaweza kukuangazia mtu aliyevunjika moyo, maskini, wafungwa au hao wanaoomboteza.
- 3) Muulize ikiwa kuna mtu maalum ama mazingira ambayo anakutaka wewe kuwapa tumaini.

Zingatia:

Baada ya kusikia sauti ya Mungu, fanya kazi pamoja ukishirikiana naye. Ukifikiria kikundi cha watu au mtu aliyemwangazia kwako, tafuta njia ya kuwafikia watu hao. Kumbuka kuwa Mungu anataka kuwaweka watu huru kiroho, kihisia na kimwili.



"Daudi* alikuwa mwanachama wa Kikundi cha Uzima cha Kambali kwenye kijiji chake. Wakati huu wa ugonjwa kanisa lake halikumtembelea kamwe, lakini Kikundi chake cha Maisha kilimtembelea na kumsaidia hadi alipofariki. Watu wa kijiji hiki wanamshukuru Mungu kwa kuwa na Kikundi hiki cha Maisha kijijini ambayo inaweza kuonyesha upendo na huduma kwa watu hata kama hawatoki kanisa moja. Roho ya mpendwa wetu ndugu Daudi ilale kwa amani."

- Ushuhuda toka Mpika, Zambia

Labda unauliza:

Je, Mungu kweli anaweza kufanya kazi kupitia mtu yeyote?

Somea tena Isaya 61:1-4 na fikiria aina ya watu ambao Mungu anasema watakuwa 'mialoni ya haki'.

Kwa rasilimali zaidi za Dignity tembelea:

www.dignityonline.org.uk/library